# Imeandikwa



JAMES KALEKWA

# IMEANDIKWA:

# *Nguvu ya neno la Mungu kukupa ushindi unaodumu*

**James & Frida Kalekwa**

Imeandikwa: *Nguvu ya neno la Mungu kukupa ushindi unaodumu.*

---

© Haki ya nakala 2016

James & Frida Kalekwa

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kutoa nakala sehemu yoyote ya kitabu kwa namna yoyote bila ruhusa ya mmiliki wa kitabu hiki isipokuwa nukuu zilizoruhusiwa kisheria

Kimetolewa na:
Kingdom Impact Publishers (KIP)
P.O Box 1074
Mwanza, Tanzania
kingdomimpactpublishers@gmail.com
+255 754 917 764
**ISBN: 978-9987-9869-9-6**

Toleo la kwanza 2016-07-28

**Kitabu hiki kimenunuliwa na:**

…………………………………………………………

…………………………………………………………

Kuwa zawadi kwa :

…………………………………………………………

…………………………………………………………

Kwaajili ya:

…………………………………………………………

…………………………………………………………

Leo Tarehe: ……/………../……………

**Mungu akubariki!**

# Orodha ya yaliyomo:

Kitabu hiki kimenunuliwa na: .......... 4

Mungu akubariki! .......... 4

Orodha ya yaliyomo: .......... 5

Shukurani .......... 7

Tunukio .......... **Error! Bookmark not defined.**

Utangulizi .......... 9

Sura ya kwanza: .......... 12

Muktadha wa andiko .......... 12

- Mawe yawe mikate .......... 15
- Darasa kwa ajili yako .......... 17
- Kumbuka: .......... 18

Sura ya Pili .......... 19

Mgeuko wa Kimtazamo .......... 19

- Mwanadamu/Mtu ni nani? .......... 20
- Vita ya kimitazamo (Paradigm war) .......... 22
- Ushuhuda wa maisha yangu .......... 25
- Kumbuka: .......... 26

Sura ya Tatu: .......... 27

Kutoka ndani kwenda nje .......... 27
Umejawa na nini ndani yako? .......... 29
Hoja ya msingi ya Yesu .......... 31
Nikiwa mwanafunzi wa shule ya upili .......... 33
Ushauri wangu binafsi .......... 34
Kumbuka: .......... 35
Mwito na Habari njema: .......... 35
Orodha ya maandiko ya msaada wa karibu: .......... 38
Kuhusu Wokovu na Msamaha wa Mungu .......... 38
Kuhusu uchumi na fedha .......... 38
Kuhusu elimu na taaluma .......... 38
Kuhusu familia na malezi ya watoto .......... 38

# Shukurani

Mwanzo hadi mwisho wa maisha yangu umo ndani ya Mungu. Hakuna namna ninaweza kuwa hivi nilivyo pasipo uwezesho wa Yesu Kristo, Roho Mtakatifu na Mungu Baba! Moyo wangu hauchoki kumshukuru Mungu kwa neema na nidhamu ya uandishi wa vitabu aliyoiweka ndani yangu.

Ninamshukuru mpenzi wa moyo wangu Frida kwa kuitia nguvu mikono yangu wakati wote wa kazi hii kubwa… Yeye ndiye tafsiri halisi ya "…wawili ni bora kuliko mmoja…"

Shukurani kwa mchungaji kiongozi wa New Vine Church (NVC), Goodluck Kyara, mlezi wangu kihuduma (mentor) ambaye ananishika mkono, kunipa nafasi na kunielekeza.

Utukufu wote uende kwa Bwana Yesu, Mungu na mwokozi wetu!

# Kutabaruku

Shauku na maombi ya moyo wangu ni kuona kanisa la Mungu linatembea na kuongozwa na misingi ya neno la Mungu na si hisia, ushabiki au mihemko.

Kitabu hiki ni maalum kwa mwili wa Kristo Yesu!

# Utangulizi

Hongera kwa kuchagua kusoma kitabu hiki na hongera sana kwa kusoma vitabu!

Msingi uliowekwa ndiyo huamua uimara wa jengo juu ya msingi huo. Iwapo mtu amekusudia kuwa na jengo litakalokaa (likakaloishi) kwa muda mrefu au kuwa na jengo kubwa au refu au lenye uzito mkubwa sana, basi mtu huyo hana uchaguzi zaidi ya kuwekeza kusimamisha msingi thabiti.

Kwenye maisha ya ukristo, kama mfumo wa maisha na si taratibu za kidini, neno la Mungu ndiyo msingi. Kila hatua ya mwamini inapaswa kuongozwa ama kuakisi kile kilichosemwa ndani ya neno la Mungu.

Binafsi, nimeshuhudia watu wakichangamka, kuhamasika na kupata joto pindi wanapokuwa kwenye makundi/makusanyiko ya wapendwa wenzao “fellowship” lakini inapofikia nyakati za kujisimami wao na nafsi zao, ndugu hao hujikuta wanayeyuka mara! Nimeshuhudia watu wakipokea uponyaji kisha baada ya muda unapotea kwa sababu “hawauamini”. Nimeona watu ambao wanakiri ahadi za Mungu na

kwa namna ya nje unaweza kushawishika ya kwamba wanaelewa wanachokifanya – kumbe la! Siyo mapenzi ya Mungu wewe uwe mkristo wa kupanda na kushuka kama jotoridi la mwili.

Baada ya kujifunza kwa watumishi kadhaa wa Mungu na kufanya tafiti kwenye machapisho mbalimbali, nimegundua ya kwamba wakristo walioweza kusimama na kujisimamia na kuacha alama ya miguu yao kwenye mchanga wa historia hawakuwa ni watu wenye ushabiki, mihemko au wenye kuzifuata hisia na misisimko… Sikuona mtu wa namna hiyo!

Wakristo waliojengwa kwenye misingi ya neno, haijalishi jambo gani liliwaijilia, bado waliweza kusimama na kujisimamia. Hata kama mazingira yalikuwa kinyume, hali hazikuwaunga mkono wala hawakua na mtu wa kuwatia moyo… bado walisimama thabiti!

Kimsingi, kila mwamini anapaswa kufikia hatua ya kuweza kusimama peke yake. Hatua hii inaweza kufikiwa iwapo tu msingi, yaani neno la Mungu litakuwa limemjaa kwa wingi ndani yake na si ile hali ya kutenda kwa kutazama wengine wanatenda nini – kufuata upepo!

Ndani ya kitabu hiki ninawasilisha mjadala na mchuano mkubwa wa kimitazamo baina ya Yesu na mjaribu ili kumsaidia mwamini kuwa na "nia (mawazo/mtazamo) ya Kristo". Ninaamini na kukuona ukichukua hatua ya kumtafuta Mungu kupitia neno lake kwa nguvu na kwa shauku kubwa kwa jina la Yesu!

James & Frida Kalekwa
Mwandishi wa kitabu
Mwanza, Tanzania

# Sura ya kwanza:

# Muktadha wa andiko

**Mathayo 4:1-4**, "Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Ibilisi. Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa. Mjaribu akamjia akamwambia, Ukiwa ndiwe mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate. Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

Moja ya wakufunzi wangu katika eneo la usomaji na kutafsiri neno la Mungu alinielekeza ya kwamba ili niwe kwenye nafasi ya kuelewa kwa upana na kuhaulisha maarifa niyapatayo kutoka kwenye andiko fulani kuja kwenye mazingira yangu ya sasa, kuna mambo ninapaswa kuyaelewa katika andiko husika: Wahusika, mazingira, nyakati, usuli, mpangilio wa kitabu na jinsi andiko lilivyopangwa (positioned).

Ili uweze kuelewa vyema andiko hili ni lazima na muhimu uelewe walau mambo kadhaa. Ninatamani

pia kuachilia uelewa huo ndani yako ili kukuza uelewa wako juu ya maandiko:

- Uhalisia wa kibaiolojia na kisayansi (scientific facts) unaonyesha ya kwamba katika hali ya kawaida mtu wa jinsia ya kiume (mwanaume) anaweza kuishi siku tano tu pasipo chakula kasha baada ya hapo ni lazima mauti imchukue. Uhalisia huo unajaribu kuelezea picha ya ujumla lakini kwenye ulimwengu wa sayansi na kanuni zake huwa kuna "*exceptions*" yaani ile hali ya kukinzana kiasi na kanuni au uhalisia fulani wa kisayansi… Kwa mfano, kuna wanaume wanaweza kukaa siku 4 au wengine siku 6 bila chakula. Ukiisoma habari ya Bwana Yesu kwa jicho la kujifunza utagundua ya kwamba, uhalisia wa kibaiolojia na kisayansi ulikuwa unaruhusu ya kwamba Yesu angekuwa amekwisha kufa tayari.

  "Akafunga **siku arobaini mchana na usiku**…." unaona ya kwamba hakuwa anapata hata nafasi ya kupata chakula kupoza njaa kwa muda wa siku arobaini?

- Uhalisia wa hali na mazingira ya wakati huo. Hebu rejea sehemu ya mwisho ya mstari wa pili "… **mwisho akaona njaa**". Utagundua ya kwamba

kabla mjaribu hajamfuata alihakikisha ya kwamba yupo kwenye hali ya uhitaji wa chakula, ndipo amfuate. Kwa hiyo, kwa namna ya kawaida unaweza kusema jaribu lilikuja kwa wakati sahihi kabisa "*perfect timing*". Kitu cha muhimu ninachotaka macho ya ufahamu wako yakione ni kwamba Yesu alikuwa kwenye hali ya uhitaji wa chakula, si kwa sababu ya hamu bali ni ile sababu ya lazima (Kuna aina mbili za kuhitaji chakula: hamu ya chakula na njaa – uhitaji wa pili huwa hauwezi kuahirishwa).

- Uhalisia wa kijiografia na kieneo. Rejea mstari wa kwanza wa andiko hili "Kisha Yesu alipandishwa na Roho **nyikani**…". Hii inatuonyesha ya kwamba kijiografia Bwana Yesu alikuwa sehemu isiyokaliwa na watu (siyo sehemu ya makazi ya watu) kwa hiyo, hakuna namna angeweza kupokea msaada wa haraka ama huduma ya kwanza kulingana na hali aliyokuwa nayo. Pia katika mazingira hayo, asingeweza kuzifikia huduma za kimsingi za kijamii kwa uharaka (he had no access to basic social services). Katika nyika hakuna huduma za matibabu, chakula wala maji na wala hakuna sehemu ambapo unaweza kulipia gharama kuzipata – hakuna huduma!

## Mawe yawe mikate

Mjaribu alipomwijia Yesu alikuja si tu kumjaribu bali kutatua matatizo yaliyokuwa yakimzunguka Yesu. Ni virahisi sana kudhani shetani ni mbaya na ana sura mbaya na mwonekano wa ajabu kwa hiyo kila analolileta ni baya sana… Ndiyo, inaweza kuwa ni ukweli lakini haikuwa hivyo kwenye jaribu hili alilotetewa Bwana Yesu.

Kugeuza mawe kuwa mikate kulikusudia kutatua maeneno matatu ambayo nimeyapembua hapo awali. Mkate ungeweza kujibu swali la kibaiolojia na kisayansi, swali la uhalisia na mazingira ya wakati huo vile vile lilikuwa ni jibu kwenye swali la uhalisia wa kijiografia na kieneo.

Binafsi, ninatamani kuondoa mtazamo wa juu juu au mwepesi ulio ndani ya wapendwa wengi ya kwamba shetani ni "mbaya" kwa hiyo wanatarajia atakuja kwa namna ya ubaya. Ukisoma maandiko vizuri hasa andiko hili utagundua ya kwamba huyu adui alikuja kuleta msaada, kutatua changamoto, kumsaidia Yesu kwenye hali aliyokuwa anaipitia. Mjaribu "*aliyafungua*" macho ya Yesu na kumwonyesha mawe ali ayageuze yawe mkate ajipatie chakula kwa ajili ya uzima wake mwenyewe. Mjaribu aliileta fursa ili Yesu aitumie

kujipatia majibu ya maswali yake matatu yaliyokuwa yakimkumba kwa wakati huo.

Kitu kingine ninachotaka ukione hapa ni ule mstari wa kwanza "Kisha Yesu **alipandishwa na Roho** nyikani…". Aliyempelekea kwenye hayo "*matatizo na changamoto*" za wakati huo alikuwa ni Roho Mtakatifu, hivyo mjaribu alitamani kutatua matatizo hayo! Mungu akusaidie uone jambo hili. Ni kama vile Roho Mtakatifu alikusudia kumuangamiza Yesu kwa kumsababisha ashinde njaa kwa muda wa siku arobaini mchana na usiku na kumuweka eneo lisilofikiwa na huduma za kijamii. Ni kama vile mjaribu alikuwa anampenda sana Yesu kiasi cha kutaka kumsaidia na kumtoa kwenye matatizo na changamoto hizo.

## Darasa kwa ajili yako

Moyoni mwangu ninawiwa kukuonyesha jambo hili kwa waziwazi na si kukuachia kulitafuta mwenyewe kwenye maelezo niliyoyatanguliza hapo awali.

Ukitazama kwa umakini utaona ya kwamba, Roho Mtakatifu alimpeleka Yesu nyikani kwa ajili ya kufunga, kukaa bila kula na kunywa, kwa muda wa siku arobaini kwa lengo la kumuandaa kwa huduma ya hadhara (public ministry) iliyokokuwa mbele yake. Tafsiri yake ni kwamba, kwa Bwana Yesu ilikuwa ni vigumu sana kuyaona na kuyafaidi matunda ya kufunga na kuomba papo kwa hapo/ wakati huo huo (immediately). Roho Mtakatifu aliratibu swala la la maombi na kufunga kimkakati, yaani, matunda yake yataonekana baada ya muda. Kwa maneno rahisi alikuwa anamuandaa Yesu kwa ajili ya kesho yake leo.

Upande wa pili, mjaribu alileta hoja za kukidhi mahitaji ya wakati huo huo (immediate gratification). Ni watu wasio na muono wa kimkakati ambao hutamani kuiandaa kesho yao ifikapo kesho. Yaani, wako radhi kugeuza " jiwe kuwa mkate" ili wapate kushiba muda huu… akili zao hupiga kelele na kusema "SASA!!!"

## Kumbuka:

- ✓ Yesu alikuwa kwenye hali ya kiuhitaji na uhalisia ulidhihirisha hivyo – kibaiolojia, kisayansi, kijiografia, kieneo, kimazingira na hali.
- ✓ Mjaribu alileta fursa ili kujibu mahitaji ya wakati ya Yesu Kristo – usidhani shetani huja kwa sura na mwonekano mbaya sana.
- ✓ Roho Mtakatifu alimpitisha Yesu nyikani kimkakati
- ✓ Andaa kesho yako leo; kidhi mahitaji yajayo sasa!

# Sura ya Pili

# Mgeuko wa Kimtazamo

Mathayo 4:4 "… **mtu** hataishi kwa mkate tu…"

Baada ya kutazama kwa upana wake muktadha wa andiko hilo, uniruhusu nikusogeze hatua nyingine katika ufahamu.

Baada ya kuwa ameletewa fursa ya kugeuza mawe kuwa mikate kwa faida ya nafsi yake mwenyewe, Yesu anajibu kwa namna ambayo huwa inanishtua sana mimi binafsi.

- Anajibu nje ya kile alichoulizwa ama mada inayozungumziwa kwa wakati huo – mjaribu anapoleta hoja ya mawe kuwa mikate, ni hoja ya chakula. Ajabu na kweli Yesu anapangua hoja hiyo kwa kuzungumzia neno la Mungu… Je, ni kwa namna gani neno linaweza kuwa katika mazungumzo ya chakula?
- Majibu ya Bwana Yesu, kwa mtazamo wa ukawaida, ni kama yamejaa uhafidhina/ushabiki

(extremism). Kimsingi, anakinzana na uhalisia na mtazamo wa kawaida wa uanadamu.

Sasa, ili uelewe vizuri alichokisema Yesu ni vyema tukarudi nyuma kidogo kutengeneza ulewa wa pamoja juu ya mwanadamu/mtu, kisha tutengeneze hatua zetu kutoka huko kuuelekea mgeuko wa kimtazamo ambao Yesu anauwasilisha kupitia majibu yake.


## Mwanadamu/Mtu ni nani?

**Mwanzo 2:7**, "Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai."

Ninachotaka kukuonyesha ni hiki: mwanadamu ni roho yenye nafsi inayoishi ndani ya mwili. Kwa hiyo huwezi kumuongelea mwanadamu kwa kutenganisha sehemu za uanadamu wake… Lazima uzungumzie roho, nafsi na mwili kwa pamoja (holistic).

Kila sehemu ya mwanadamu huwa na chakula chake kulingana na asili na utendaji wake. Mwili hula vyakula vya wanga, vitamini, mafuta, maji n.k ili uwe na afya

na utende sawasawa. Wakati nafsi hula taarifa kupitia milango mitano ya fahamu na roho hula ibada. Ndani ya kila mwanadamu huwa kuna shauku isiyoweza kuelezeka juu ya uhitaji wa kushirikiana na ulimwengu wa juu/roho (longing to communion with the supernatural realm). Kila mwanadamu ana hilo ombwe (vacuum) ndani yake ambalo hukidhiwa na ibada tu. Swala la nani anamwabudu nani hiyo ni hoja nyingine, lakini itoshe tu kukujulisha ya kwamba mwandamu huilisha roho yake ibada.




**Taswira 1**. Sehemu za mwanadamu na vyakula vyake.

## Vita ya kimitazamo (Paradigm war)

Baada ya kuwa umemuelewa mwanadamu kwa mtazamo mpana (holistic perspetive) sawa sawa na neno la Mungu, naomba kwa miwani hiyo tuyarejelee mazungumzo baina ya Yesu na mjaribu.

Kwenye mjadala hu, ambao mimi binafsi huwa ninaona vita kali sana ya kimitazamo, utagundua mjaribu anamwendea Yesu na kumwambia: "… amuru kwamba mawe haya yawe mikate…" kisha kwenye mstari wa nne tunaona majibu ya Bwana Yesu "…mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

Hebu nikuonyeshe hii mitazamo inayokinzana kwenye mjadala huu kisha tupate wasaa wa kuchanganua mambo:

- Shetani alilenga kukidhi mahitaji ya Sehemu moja tu ya mwanadamu, yaani mwili (mkate ni chakula cha mwili peke yake) wakati Yesu alileta hoja ya kulisha roho na nafsi – "… bali kwa **kila neno**"… neno ni aina na njia mojawapo ya uwasilishaji wa taarifa/habari. Pili, Yesu anasema "…litokalo katika **kinywa cha Mungu**." anazungumzia asili

ya hilo neno! Asili yake ni Mungu – hapa ninamaanisha siyo tu kwamba anayeliachilia neno hilo ni Mungu bali aliyeliumba neno hilo ni Mungu na linatokana naye!

Mfano: Bidhaa inaweza kutolewa na ndugu kutoka Mwanza, Tanzania. Ilhali bidhaa hiyo hutengenezwa au hutokana na mkoa wa Mtwara. Yaani unaweza ukapokea zawadi ya vinyago kutoka Mwanza lakini asili ya vinyago hivyo ni Mtwara.

Ninachotaka kukuonyesha ni kwamba Yesu hakukusudia kumweleza shetani ya kwamba neno hilo linatoka kwa Mungu bali pia linatokana (asili) na Mungu… Ningekuwa ninafundisha kwa lugha ya kiingereza ningeweza kusema "… not only that the word is from God but also it is of God…"

Hii inatuongezea ushahidi ya kwamba Yesu anatambulisha ile shauku ya kila mwanadamu kuugusa/kushirikiana na ulimwengu wa roho.

Kwa mantiki hiyo basi, Yesu alikuwa akipiga vita sana mtazamo wa kishetani wa kushughulika na mahitaji ya mwanadamu kwa upande mmoja tu bila kumhudumia mwanadamu kwa ukamilifu wake!

- Yesu anaonyesha kutambua kazi ya chakula kwenye mwili lakini hauoni huo kuwa ndiyo mwisho bali anaamua kuyatanua mawazo na kuyapeleka nje ya boksi. "… mtu hataishi kwa makate **tu**…". Ukitazama kwa umakini utang'amua ya kwamba Bwana Yesu hakuifutilia mbali hoja ya mkate moja kwa moja bali alionyesha inahitaji kujazilizwa. Yesu hasemi "mtu hataishi kwa mkate…" bali twaona anaongeza neno "tu"! Ninaamini Biblia yako imeandikwa hivyo pia. Hilo neno "tu" ni ishara ya kutambua ya kwamba mkate ni kwa ajili ya mwili wa mwanadamu, lakini haishii hapo, ndipo anaamua kutukaribisha kwenye viwango vya juu vya kumtazama mwanadamu.
- Yesu anatambulisha vipaumbele katika ujenzi wa maisha kamilifu ya mwanadamu. Ili mtu aweze kusimama na kuacha alama ya miguu kwenye mchanga wa historia (footprint on the sand of history), kuna namna ambayo mtu huyo anapaswa kujengwa/kustawi… Kukua/kustawi kutoka ndani kwenda nje (inside-out) wala si kutoka nje kwenda ndani (outside-in) – nitalijadili hili katika sura inayofuatia.

## Ushuhuda wa maisha yangu

Katika ukuaji wangu ndani ya wokovu, nilianza kupata mwongozo wa kiungu ndani yangu kuhusu maisha yangu ya utumishi hasa eneo la kuzalisha maarifa. Katika umri wa miaka kumi na kitu nilianza kujibidiisha kutafuta maarifa nikiamini ya kwamba yananiandaa kufikia maono. Nilifikia hatua ya kuchagua kutembea kwa miguu badala ya kupanda usafiri wa umma na kutunza (saving) pesa niliyopewa na wazazi wangu ili niweze kununua vitabu. Nikiwa chuo kikuu, nikisomea shahada ya kwanza ya Sosholojia, niliweza kutumia sehemu kubwa sana ya pesa yangu na muda wangu mwingi kununua vitabu na mikanda ya video (DVD) ya mafundisho. Inawezekana kabisa nilikuwa miongoni mwa wanafunzi wachache wa vyuo vikuu walio na shubaka la vitabu na vitabu vingi ndani yake. Moyo wangu ulishawishika mapema sana ya kwamba kwa kuiandaa roho na nafsi yangu, siku za usoni nitaweza kuenenda kwa urahisi sana kwenye maono na hasa eneo la uandishi wa vitabu.

Haikunisumbua hata kidogo kutoa pesa kununua vitabu vyenye gharama ya shilingi 50,000 -100,000

(elfu hamsini mpaka laki moja) kwa kitabu kimoja kwani nilikuwa nina uhakika na utendaji wa kujijenga ndani ili kuyaathiri mambo ya nje.

Nilijifunza kanuni hii anayoisema Bwana Yesu… Kwa maneno yangu binafsi huwa ninapenda kujisemea "Mimi James sitaishi kwa mkate, matunda, wali, mboga mboga, maji (unaweza kuongeza orodha wa vyakula) TU, bali kwa KILA NENO litokalo katika kinywa cha MUNGU."

## Kumbuka:

- ✓ Mwanadamu ni roho yenye nafsi inayoishi ndani ya mwili – kila sehemu ya mwanadamu ina chakula chake.
- ✓ Mtazamo wa kiungu ni kukutana na mahitaji ya sehemu zote za mwanadamu (holistic perspective)
- ✓ Mtu mkomavu na mwenye kutenda mambo makuu kwenye maisha hujengwa/hustawi kutoka ndani kwenda nje (Inside-out)

# Sura ya Tatu:

# Kutoka ndani kwenda nje

Kila ukionacho kikijidhihirisha kwenye maisha ya mwanadamu yeyote ni matokeo ya kile kinachoendelea ndani yake. Maisha yanayoonekana ni matokeo ya maisha yasiyoonekana yaliyo ndani ya mtu. Ndiyo kusema kile ukionacho ni matokeo tu!

Kila usomapo kitabu hiki na kukutana na neno "ndani" ninatamani uelewe ni mjumuisho wa mambo yafuatayo: mitazamo, imani, uelewa, mfumo fikra, maoni n.k ambavyo hutokana na kile mtu alichowahi kusikia, kuona, kusoma, kusimuliwa, kuaminishwa na kuamini.

Kwa ujumla wake mambo haya ndiyo ambayo huamua mwenendo wa maisha ya mtu. Haijalishi ameokoka au la, bali inategemea "ndani" yake amebeba nini.

Kitu anachokizungumza Yesu ili kujibu hoja za yule mjaribu kimebeba mantiki hiyo. "...mtu hataishi kwa

mkate tu; bali (ataishi) kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu." . Tafsiri yake ni kwamba "neno" linauwezo wa kusababisha maisha ya mwanadamu yeyote kusonga mbele, na si mkate (chakula) peke yake kama vile ambavyo mjaribu (na watu wengi) hudhani.

Unaweza kulitazama jambo hili kwa nanmna hii, chakula kupitia mfumo wa umeng'enyaji, ndiyo husababisha mwili wa mwanadamu kuwa vile ulivyo. Kama huwa unafuatilia maswala ya afya na chakula utakubaliana nami ya kwamba kuna vyakula ambavyo huupatia mwili nguvu, vipo viletavyo joto kwenye mwili, vipo vyenye kazi ya kuulinda mwili, vipo vinahusika na ukuaji na uimarishaji wa mifupa na kucha n.k. Hivyo basi, ukiouna mwili wa mwanadamu uko njiani uwe na uhakika umekiona chakula! Kwa maana ya uelewa huo, mwili wa mwanadamu ni chakula!

Yesu anajibu hoja ya mkate kwa hoja ya neno la Mungu. Kwa haraka unaweza kudhania vitu hivi havina uhusiano wowote. Maadamu Yesu ametumia neno la Mungu mahala pa mkate, ni hekima kutaka kutafuta kujua uhusiano uliopo.

Neno la Mungu, ni chakula kwenye roho na nafsi ya mwanadamu! Kiutendaji, mwanadamu huakisi ni kwa kiasi gani amejawa neno la Mungu ndani yake.

## Umejawa na nini ndani yako?

Hebu nikuonyeshe jambo hili kwenye neno la Mungu ili kuinua uelewa wako.

**Mithali 4:23**, "Linda moyo wako kuliko yote uyalindayo; Maana ndiko zitokako chemchemi za uzima."

Neno la Mungu linatuagiza kulinda sana moyo na sababu pekee inayotolewa na juu ya agizo hili ni kwamba "…ndiko **zitokako** chemchemi za uzima". Kwa hiyo, uzima wa maisha ya mtu hutokea ndani ya moyo wake. Kwenye moyo wa mtu ndiko iliko hazina ya maisha yake yote. Kama huwa unatunza pesa kwenye benki au taasisi yoyote ya kifedha, natambua unajua ya kwamba kinachoamua uchukue kiasi gani kutoka kwenye hazina yako ni kile kilichomo ndani ya hazina hiyo na siyo uhitaji wako binafsi. Hebu nikutazamishe tena eneo jingine.

**3Yohana 1:2**, "Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, **kama vile** roho yako ifanikiwavyo."

Neno la Mungu linaiweka kanuni hii ya mafanikio ya kwamba mambo yote na afya yako yanaamuliwa na mafanikio ya roho yako "…kama vile…" yaani kwa kiwango, kiasi, kasi, mwenendo uleule wa roho yako.

Kitu kinachotambulishwa na neno la Mungu ni kwamba hatuwezi kufanikiwa zaidi ya vile tunavyofanikiwa ndani yaetu! Mungu akusaidie kukamata jambo hili kwa wepesi.

Je, umegundua neno la Mungu halijatenganisha maeneo baadhi ya kimaisha ambayo huamuliwa na mafanikio ya ndani? Umegundua hilo? "… ufanikiwe katika mambo yote…" Maana yake ni kwamba hakuna hata eneo moja ambalo unaweza kupiga hatua yoyote ya maana pasipo msaada wa neno la Mungu kufanikisha roho yako.

Uniruhusu nikuchukue kwenye andiko jingeni tena ili tujifunze pamoja.

**Mithali 23:7a**, "Maana aonavyo nafsini mwake, ndivyo alivyo…."

Kitu ninachotaka kusisistiza kwako ni kwamba uko jinsi ulivyo kwa sababu ya vile ulivyo ndani yako. Kwa mantiki hiyo basi, kinachoanza kufanikiwa, kustawi,

kukua, kuendelea ni "ndani" mwako kisha mafanikio hayo ya ndani huanza kujidhihirisha kwa nje.

Kuna wakati Yesu alifundisha jambo ambalo linaakisi kanuni hii:

**Mathayo 12:35**,"Mtu mwema katika akiba njema hutoa mema; na mtu mbaya katika akiba mbaya hutoa mabaya."

Swali kwako, umejaza nini ndani yako? Umejawa na taarifa gani? Umejawa na ibada gani? Hazina hiyo uliyoitunza ndani yako ndiyo huamua jinsi ulivyo sasa! Huwezi kutoa tofauti na ulichowekeza ndani yako.

## Hoja ya msingi ya Yesu

Yesu anamjibu mjaribu ya kwamba "mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu" Hii inatupa kutambua ya kwamba Yesu alikuwa akitembea na kanuni kubwa za maisha (principle-centred). Anajenga hoja mbele ya mjaribu ya kwamba kile kilichomo ndani ya mwanadamu ndiyo huamua mwenendo wa maisha. Yaani, kujawa

na neno la Mungu, ndiyo huamua nini kitokee kwenye maisha ya nje.

Wakati mjaribu alikusudia kujenga hoja na kuisimamia ya kwamba iwapo Yesu (mtu) atakula "mkate/chakula", shibe ya mwili itaamua hali (status) yake ya ndani! Hiyo ndiyo huitwa nje kwenda ndani (outside-in)… Hakuna matokeo yadumuyo katika hiyo!

Hebu nikuonyeshe eneo moja kwenye maandiko matakatifu:

**Mwanzo 3:4-5**, "Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya."

Hawa ndugu wapenzi, waliumbwa kwa mfano (mfanano wa Mungu) na walikuwa na ushirika wa karibu na Mungu – hiyo inaonyesha hali (status) yao ya ndani. Ajabu na kushangaza, mjaribu anawajia na kuwahakikisha kuongeza viwango vya ndani – watakuwa kama Mungu! Lakini njia anayowaambia kuitumia ili kuathiri maisha yao ya ndani ni ile ya kutokea nje kwenda ndani (outside-in). Walipaswa

kula tunda (kama ilivyokuwa mkate wakati wa Yesu) – kimsingi hicho ni chakula. Na kwa kula chakula hicho hali yao ya ndani itabadilika na kupanda kwenda viwango vikubwa zaidi… Kilichotokea ni anguko kubwa, kufukuzwa Edeni, kupoteza ushirika na Mungu na kuleta laana kwenye uzao!

Huo ni ushahidi ya kwamba njia hiyo alishawahi kuleta madhara makubwa sana kwa wanadamu na hivyo isingeweza kuleta matokeo mazuri kwa Yesu pia! Ndiyo hasa msingi wa hoja ya Yesu "…ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

## Nikiwa mwanafunzi wa shule ya upili

Nilipookoka nikiwa ninasoma shule ya upili jijini Mwanza iitwayo Mwanza Baptist Secondary School, kuna baadhi ya waalimu wangu wazuri na wenye kunipenda sana walijaribu kunishauri kuachana na mambo ya kuokoka kwa vile wao wamekwishaona madhara yake wakiwa shuleni na vyuoni. Baada ya ushauri kutofanikiwa, walianza kutumia njia ya "*name and shame*". Kunitaja (mimi na ndugu wengine waliookoka) mbele ya umati na kuanza kudhihaki na

kuniaibisha. Ukweli ni kwamba, madai ya waalimu wangu yalikuwa na uhalisia (facts). Ni kweli wanafunzi wengi waliookoka walikuwa hawafanyi vizuri sana kwenye masomo na huo ulikuwa ushahidi ya kwamba ningeelekea huko pia. Ashukuriwe Mungu nilijibidiisha kutafuta mafundisho hasa yahusianayo na elimu na maneno yaliyotamkwa kinyume na mimi. Mpaka ninahitimu masomo yangu katika shule hiyo, kutofaulu kimasomo ilikuwa ni hadithi tu iliyoshindwa kutimilika kwenye maisha yangu! Utukufu kwa Bwana Yesu!

## Ushauri wangu binafsi

Ili uone ustawi katika maeneo mbali mbali ya kimaisha, ninakushauri utafute maarifa ya Mungu kuhusiana na eneo husika. Unaweza kujikuta unakutana na uangamivu kwenye eneo fulani la kimaisha kwa sababu "watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa…". Kuokoka ni mtaji, kwa hiyo unapaswa kuukuza mtaji wako katika maeneo yote ya kimaisha ili upate matokeo yadumuyo. Usikae chini wala usikae kimya kusikiliza maoni ya watu au vikundi

binafsi, bali tafuta neno la Mungu ili liwe msimamo wa maisha yako… Kwa sababu "IMEANDIKWA…"

## Kumbuka:

- ✓ Maisha ya nje ni udhihirisho wa kinachoendelea ndani ya mtu.
- ✓ Katika maeneo mbalimbali ya kimaisha mtu huanza kufanikiwa ndani yake kisha mafanikio hayo huamua mafanikio ya nje.
- ✓ Kiwango cha neno ndani ya mtu katika Nyanja fulani ndiyo huamua kiwango cha mfanikio huko.

## Mwito na Habari njema:

Sikutamani kuhitimisha kitabu hiki pasipo kukushirikisha ukweli ya kwamba kama haupendi hali uliyo nayo sasa kwa ujumla au katika eneo fulani la kimaisha, basi usife moyo, mambo yanaweza kubadilika na kubadilishwa! Tumia muda wako kujifunza neno la Mungu yaani Biblia na mafundisho ya neno la Mungu kupitia machapisho au namna zingine.

Pili, kama haujaokoka na moyoni mwako ungetamani kuona mafundisho haya yanafanyika halisi kwenye maisha yako. Huhitaji kujidanganya nafsi yako, jisalimishe kwa Yesu Kristo upate mwanzo wa usalama kamili wa maisha. Kuokoka si habari ya dini, bali ni kuwa na uhusiano binafsi na Mungu. Kama unahitaji kufanya hivyo, tafadhali chukua maneno haya na uyaseme kwa kumaanisha kutoka moyoni mwako:

**Baba Mungu, asante kwa kunipenda ningali mwenye dhambi. Nimesikia neno lako na kutambua ya kwamba mimi ni mwenye dhambi hivyo ninatubu dhambi zangu zote nilizokutenda kwa mawazo, maneno na kwa matendo. Nina amini kwamba Yesu Kristo alikufa msalabani kwaajili yangu na kwamba yu hai kutoka kwa wafu. Muda huu ninamkabidhi Yesu Kristo maisha yangu, awe Bwana na mwokozi wa maisha yangu tangu sasa na maisha yangu yote.**

**Asante Yesu kwa kuniokoa na kunipa uzima wa milele. Ninaomba kupitia Jina la Yesu Kristo mwana wa Mungu aliye hai. Amina!**

Kama umesali sala hiyo, hongera kwa kuwa sasa umeokoka!

Tafadhali uwe huru kutushirikisha juu ya uamuzi wako wa kumfuata Yesu (Uamuzi bora kabisa ambao mtu mwenye akili timamu anaweza kuufanya duniani). Iwapo kuna ushuhuda wowote utokanao na usomaji wa vitabu vyetu, au iwapo unataka kujua namna unaweza kupata matoleo mengine ya vitabu au hitaji la maombi au jambo lolote. Tushirikishe kwa mawasiliano yafutayo:


Kingdom Impact Publishers

P.O. Box 1074

Mwanza, Tanzania

Email: kingdomimpactpublishers@gmail.com

Simu: +255 754 917 764

## Orodha ya maandiko ya msaada wa karibu:

**Kuhusu Wokovu na Msamaha wa Mungu**
Yohana 3:16-21; Yohana 15:13; Warumi 10:9-10; 1 Yohana 1:9; Matendo 4:12; Wakolosai 2:14-15; Yohana 1:12; Warumi 1:16; 2 Wakorintho 5:17; Waefeso 2:8-9

**Kuhusu uchumi na fedha**
2Korintho 8:9; Kumb 8:18; Mithali 13:11; Mithali 12:27; Mhubiri 7:12; Mithali 18:11; Wafilipi 4:19; Malaki 3:10-12; Mithali 10:4; Mithali 3:9-10

**Kuhusu elimu na taaluma**
Mithali 4:13; Danieli 1:20; Zaburi 119:99; Mithali 1:7; Isaya 28:9-10; Mithali 16:16; Mithali 9:10

**Kuhusu familia na malezi ya watoto**
Waefeso 5:25-31; 1Timotheo 5:8; Mithali 17:6; Zaburi 127: 3-5; Waefeso 5:22-24; Waefeso 6:1-4; Mithali 15:17; Mithali 22:6

# KUHUSU MWANDISHI



**James Kalekwa** ni amemwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma.


James Kalekwa

james_kalekwa

@MchungajiJK

+255 754 917 764